JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MKUU WA MKOA WA RUVUMA





# JARIDA LA RS RUVUMA

## TOLEO LA KWANZA MEI 2024





www.ruvuma.go.tz



## KARIBU MKOA WA RUVUMA

Haki zote zimehifadhiwa.Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupigachapa, kutoa nakala kivuli au kutoa baadhi ya maandishi ya Jarida hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Mwandishi kwa maandishi.

## JARIDA LA RS RUVUMA TOLEO LA KWANZA MWEZI MEI 2024

Jarida limehaririwa na **Albano Midelo** wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

# YALIYOMO

1.Tamasha la utamaduni la kitaifa kufanyika Songea
2.Serikali ilivyowakomboa wananchi wa Mpitimbi
3.Bwawa la Mpitimbi kivutio kipya cha uwekezaji
4.Watahiniwa 4,521 kufanya mtihani wa kidato cha sita Ruvuma
5.Serikali yatoa bilioni 2.5 kwa TANROADS kurejesha miundombinu
6.Luteni Kanali Mstaafu wa Songea aliyesoma na Idd Amin afariki Dunia
7.Waziri Mhagama awafunda wazazi kuhusu malezi bora
8.Madaktari bingwa 40 waanza kutoa huduma za kibingwa Ruvuma
9.Waziri Mhagama azindua mradi wa bilioni 3.1 Songea
10.TANROADS yakamilisha kazi ya kuimarisha daraja la Muhuwesi
11.Milioni 302 zaboresha mazingira ya kufundishia wenye ulemavu Tunduru
12.Wananchi Ruvuma kunufaika na huduma za matibabu ya kibingwa
13.Maadhimisho ya kimataifa ya familia kufanyika Namtumbo
14.Serikali yatoa milioni 434 kujenga stendi mpya Peramiho
15.Soko la madini Tunduru kufanyika eneo moja
16.WWF kuboresha uhifadhi na utalii Ruvuma
17.Mbunge wa Madaba awapiga jeki wanafunzi wa Lilondo
18.Serikali yatoa magari mawili ya magonjwa Madaba
19.TAKUKURU Ruvuma ilivyochunguza miradi 15 ya bilioni 10
20.Serikali yaboresha majengo ya hospitali ya Tunduru
21.Watumishi Ruvuma walivyoadhimisha Mei Mosi Tunduru
22.RC Ruvuma awaapisha wajumbe wa Baraza la Ardhi
23.Madaktari bingwa waweka kambi ya siku tano HOMSO
24.Maadhimisho ya siku ya mkulima Namtumbo
25.Ruvuma kituo cha pili kwa ukubwa uzalishaji mbegu bora nchini
26.Wawekezaji wanakaribishwa Ruvuma
27.Uvuvi unavyochangia mapato kwa wananchi Nyasa
28.Shamba la mbegu bora kuimarisha sekta ya kilimo Ruvuma

# TAHARIRI

Wapendwa wasomaji wetu ninayoheshima kubwa kuwaalika katika Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kusoma habari na makala mbalimbali ambazo zinakuwa zinachapishwa na jarida hili.
Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia kitengo cha Mawasiliano Serikali kuhakikisha kila mwezi GCU Mkoa na Halmashauri zake zinachapisha jarida ili kutangaza shughuli mbalimbali zinazofanywa na serikali ikiwemo kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, mahusiano na kutangaza fursa za utalii na uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma na namna viongozi wanavyosikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Furahia kusoma

## TAMASHA LA UTAMADUNI LA KITAIFA KUFANYIKA JULAI UWANJA WA MAJIMAJI SONGEA



TAMASHA la Utamaduni la Kitaifa la tatu linatarajia kufanyika kwenye uwanja wa Majimaji mjini Songea mkoani Ruvuma kuanzia Julai 20 hadi 27 mwaka huu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Tamasha hilo Joel Mbewa amesema tamasha la kwanza la kitaifa la utamaduni lilifanyika mkoani Dar es salaam mwaka 2022 na tamasha la pili lilifanyika mkoani Njombe mwaka 2023.

Amesema katika matamasha hayo mawili ya kitaifa Mkoa wa Ruvuma ulifanikiwa kushika nafasi ya sita kitaifa kati ya mikoa 31 ya Tanzania Bara na visiwani.

“Kwa kuwa tamasha hili mwaka huu kitaifa linafanyika mkoani Ruvuma,tumedhamiria kufanya vizuri Zaidi ikiwezekana kushika nafasi ya kwanza kitaifa kati ya mikoa 31 inayoshiriki kwenye tamasha hilo’’,alisisitiza.

Tamasha la kitaifa la utamaduni lilianzishwa mwaka 2022 ikiwa ni kutekeleza kwa vitendo maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa alipokuwa mgeni rasmi mkoani Mwanza Septemba 8,2021 katika Tamasha la utamaduni la Bulabo.

Rais Samia aliagiza matamasha ya utamaduni kufanyika kwa mzunguko kila Mkoa ili watanzania wajue mila na desturi za kila Mkoa ambapo aliagiza kuwe na mashindano ya ngoma za asili na washindi wapewe Tuzo.

Malengo makuu ya tamasha la kitaifa la utamaduni ni kurithisha amali za utamaduni kwa vitendo, kuchochea maendeleo ya utalii wa kiutamaduni, Sanaa za asili,sekta za ubunifu wa asili, kuhamasisha utaifa,uzalendo na urithishaji wa maadili kwa mtanzania

## SERIKALI YAWAKOMBOA WANANCHI WA MPITIMBI



Serikali imewaondolea adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya wananchi wa Kata ya Mpitimbi Halmashauri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma baada ya kuboresha huduma za afya katika hospitali ya Halmashauri hiyo iliyojengwa Kijiji cha Mpitimbi.

Mbunge wa Jimbo la Peramiho ambaye pia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Sera,Bunge na Uratibu  Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa niaba ya wananchi wa Mpitimbi amemshukuru Rais Samia kwa kutoa fedha za kutekeleza mradi huo.

“Nainua sauti ya moyo wa shukrani kwa Rais Samia kwa sababu kata ya Mpitimbi haikuwahi kuwa na ndoto ya kujengewa hospitali kubwa ya Wilaya’’,alisema.

Amesema wananchi wa  Kata ya Mpitimbi na Tarafa ya Muhukuru matibabu yao ya kibingwa ilikuwa ni lazima wayapate kwenye hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea au Kwenda kwenye hospitali ya Rufaa ya Misheni ya Mtakatifu Joseph Peramiho.

Amesema Jimbo la Peramiho lina kata saba katika Tarafa ya Muhukuru ambazo sasa zitakuwa zinapata huduma za matibabu katika hospitali ya Mpitimbi na kwamba hospitali hiyo pia inatoa huduma kwa wananchi wa nchi Jirani ya Msumbiji ambao wanapakana na Jimbo la Peramiho katika Kijiji cha Mkenda kilichopo mpakani mwa Tanzania na Msumbiji.

Amesema serikali imeboresha majengo na kununua vifaa tiba vya kisasa ambavyo vinawezesha huduma za matibabu za kibingwa kutolewa katika hospitali hiyo.

Amesema madaktari bingwa wamefika katika hospitali hiyo kutoa huduma mbalimbali za kibingwa ambao wameanza kutoa huduma hizo kuanzia Mei 6 hadi 10 mwaka huu hivyo kutoa fursa kwa wananchi wa vijijini kupata huduma za matibabu za kibingwa.

Cathibet Mapunda Mkazi wa Kijiji cha Mpitimbi aliyekuwa na changamoto ya usikivu  ameipongeza serikali kwa kuwapeleka madaktari bingwa katika hospitali hiyo ambapo ameweza kupata huduma za kibingwa na hivi sasa hali yake imerejea kama kawaida.



## BWAWA LA MPITIMBI KIVUTIO KIPYA CHA UWEKEZAJI SONGEA



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Mheshimiwa Jenista Mhagama ameagiza kuboreshwa Bwawa la maji la asili lililopo katika Kijiji cha Mpitimbi wilayani Songea mkoani Ruvuma ili liingizwe kwenye mpango ufugaji endelevu wa viumbemaji.

Waziri Mhagama amesema hayo wakati anazindua mradi wa kuimarisha lishe na ufugaji endelevu wa viumbemaji kwa wakulima wadogo uliofanyika Kijiji cha Mpitimbi wilayani Songea.

Katika mradi huo serikali kupitia shirika la IFAD imetenga kiasi cha shilingi bilioni 3.1 kutekeleza mradi huo katika wilaya za Songea na Mbinga mkoani Ruvuma na Wilaya za Ruangwa na Mtama mkoani Lindi,mradi ambao unatekelezwa kwa miaka miwili kuanzia Machi 2024 hadi Machi 2026.

“kuna bwawa la Mungu linalovutia sana lipo hapa Mpitimbi tena lipo njiani tu mnaweza kujionea ili kuangalia namna mnavyoweza kulitumia bwawa hilo la asili lenye ukubwa wa hekta 17 lenye uwezo wa kuingia samaki wengi kama litaboreshwa vizuri’’,alisisitiza Mhagama.

Mbunge huyo wa Peramiho amesema wamedhamiria kuiona Mpitimbi inakuwa kituo kikubwa cha ufugaji wa Samaki baada ya kuboresha bwawa hilo ambalo litakuwa kivutio kwa wawekezaji na chanzo kikubwa cha mapato na lishe bora kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma

Mhagama amesema Bwawa hilo ni kivutio kikubwa kwa wageni wengi pia linaweza kusaidia mradi huu wa ufugaji endelevu wa viumbemaji wakiwemo samaki ambapo Serikali ya Rais Samia imewekeza mabilioni ya fedha kutekeleza mradi huu.

Waziri Mhagama amebainisha kuwa wameanza kuteta na Mwakilishi wa Shirika la IFAD ili mradi wa bwawa la asili Mpitimbi uende sanjari na mradi wa shamba darasa la ufugaji Samaki lililopo Kijiji cha Mpitimbi

## WATAHINIWA 4,521 KUFANYA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA RUVUMA



JUMLA ya watahiniwa 4,521 wamesajiliwa kufanya mtihani wa kidato cha sita 2024 mkoani Ruvuma ambao umeanza Mei 6,2024 na unatarajia kukamilika Mei 24 mwaka huu.

Afisa Elimu wa Mkoa wa Ruvuma Mwl. Edith Mpinzile amesema kati ya watahiniwa hao watahiniwa wa shule ni 4,313 na watahiniwa wa kujitegemea ni 208.

Amewataja watahiniwa wa Ualimu waliosajiriwa na na kufanya mtihani wa Ualimu ni 187 ambao wanatoka katika vyuo vya ualimu Songea na chuo cha Ualimu Nazareti kilichopo Mbinga.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed anawatakiwa watahiniwa wote wa Mkoa wa Ruvuma mtihani mwema wa kidato cha sita 2024 na ualimu.

Nchini Tanzania Jumla ya watahiniwa 113,504 wa kidato cha sita na ualimu ngazi ya cheti na stashahada wanafanya mitihani yao kuanzia Mei 6 hadi 24 mwaka huu .

Mtihani huo wa kidato cha sita unafanyika katika shule 931 na vituo vya watahiniwa wa kujitegemea 258

## SERIKALI YATOA BILIONI 2.5 KWA TANROADS KUREJESHA MIUNDOMBINU



WAKALA wa barabara (TANROADS) Mkoa wa Ruvuma,umepokea Sh.bilioni 2.5 kati ya Sh.bilioni 6 ilizoomba ili kurejesha miundombinu ya barabara zilizoharibiwa na mvua za masika katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Hayo yamesemwa na Meneja wa TANROADS Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Saleh

Juma,baada ya kukagua kazi ya urejeshaji wa miundombinu ya daraja la Mto maarufu la Namiungo wilayani Tunduru.

Saleh, amemshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan,kwa kuidhinisha fedha hizo ambazo zitatumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara kwenye maeneo yenye changamoto ili kutoa fursa kwa shughuli za usafiri na usafirishaji kuendelea kama kawaida.

Amesema,licha ya mvua za masika kunyesha kwa wingi katika Mkoa Ruvuma,barabara zote zilizo chini ya TANROADS zinapitika na hakuna shughuli za kijamii zilizosimama kutokana na ubovu wa barabara.

Mwezi Machi mwaka huu daraja la Namiungo lilipata athari kubwa baada ya maji ya mvua kupita juu ya daraja na kuharibu miundombinu,hali iliyosababisha magari kupita upande mmoja.

Meneja huyo wa TANROADS Mkoa wa Ruvuma amesema,kazi ya kurejesha miundombinu ya daraja hilo imechelewa kukamilika kutokana na changamoto ya mvua, ambapo magari ya mkandarasi yameshindwa kufika maeneo yanakopatikana mawe na vifusi.

Hata hivyo,amemtaka mkandarasi kuhakikisha anakamilisha kazi mwishoni mwa mwezi huu ili barabara hiyo irudi kwenye hali yake na wananchi waendelee kuitumia katika shughuli zao za uzalishaji mali.

Mhandisi wa kampuni ya Ovans Constructions Ltd iliyopewa kazi ya matengenezo ya daraja la Namiungo Azimio Mwapongo amesema,amehaidi kufanya kazi usiku na mchana ili waweze kukamilisha kazi mwisho wa mwezi huu.

**LUTENI KANALI MSTAAFU WA SONGEA ALIYESOMA NA IDD AMINI WA UGANDA AFARIKI DUNIA**




Tanzania haitamsahau Dikteta Idd Amini Dada aliyeitawala Uganda kwa mabavu kisha kuvamia Tanzania mwaka 1978 ambapo Tanzania iliingia vitani na kufanikiwa kumng'oa mvamizi huyo mwaka 1979.

Luteni Kanali Mstaafu Daniel Gangisa (97) pichani kulia akiwa na rafiki yake Dikteta Idd Amini Dada amefariki Dunia Mei 6,2024 nyumbani kwake Chandarua Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma,maziko ya mpiganaji huyo yanatarajia kufanyika kijeshi Mei 10 nyumbani kwake Chandarua .

Akihojiwa na mwandishi wa Makala haya wakati wa uhai wake Luteni kanali Mstaafu Gangisa anasema anamfahamu vizuri Dikteta Idd Ami kwa sababu walisoma na kufanyakazi pamoja kwa miaka mitatu Nakuru nchini Kenya.

Gangisa alizawaliwa mwaka 1927 katika eneo la Ruhuwiko mjini Songea ambapo alijiunga na jeshi la wakoloni mwaka 1947 ambapo mwaka 1953 alikwenda chuo cha Jeshi Nakuru Nchini Kenya ili kupata mafunzo Zaidi ya kijeshi ambako alikutana na Dikteta Idi Amini.

"Nimesoma na Idd Amini miaka mitatu kuanzia 1953 hadi 1955 alikuwa rafiki yangu sana,tulikuwa tunalala chumba kimoja bwenini, baada ya kumaliza kozi mimi na Amini tulipata alama za juu hivyo chuo kilitupa mkataba wa kuwa walimu

tulifanya kazi sote tukiwa na cheo cha Sajenti kwa miaka mitatu'',anasema Luteni Kanali Mstaafu Gangisa.

Hata hivyo Gangisa anasema licha ya Amini katika kipindi hicho kuonekana kuwa ni kijana mtulivu na ambaye hakuwa mgomvi sana isipokuwa alikuwa mpiganaji wa ngumi na kwamba Amin alimwomba Gangisa amfundishe ngumi,lakini alikataa.

Gangisa anasema kwa muda alioishi na Idd Amin aligundua dosari kubwa aliyokuwa nayo tangu kipindi hicho Dikteta Idd Amin alipenda sana vyeo hata aliposikia amepindua nchi hakushangaa kwa sababu alimfahamu.

Luteni Kanali Mstaafu Gangisa anasema baada ya kumaliza mkataba wa kufundisha Nakuru alirudi Nyeri nchini Kenya kambi yake ya Jeshi kuendelea na Vita ya Maumau kisha alikwenda kwenye vita nchini Mauritius na Idd Amin alirudi kwao Uganda ambapo mara ya mwisho kuonana na Idd Amin anasema ilikuwa mwaka 1960 nchini Kenya.

Anasema mwaka 1964 alishiriki katika kuunda JWTZ Jeshi jipya lenye heshima nchini Tanzania na kwamba yeye ni miongoni mwa maafisa waliunda JWTZ ambapo yeye ni Ofisa wa 50 wakati huo akiwa na cheo cha Luteni Kanali.

Kwa mujibu wa Luteni Kanali Mstaafu huyo,Hayati Baba wa Taifa Mwl. Julius Nyerere wakati anaanza harakati za uhuru na kuunda chama cha TANU yeye alikuwa na Idd Amini Nakuru Kenya.

"Idd Amini ndiye aliyenipa taarifa kwamba wewe Mswahili nyumbani kwako kuna bwana ameanzisha Chama cha kupigania uhuru,alinitisha kwamba MAUMAU itaamia kwetu,nikamwambia Mungu yupo,alikuwa anaongea Kiswahili kizuri,alikuwa rafiki yangu mkubwa sana'',alisisitiza Gangisa.

Gangisa aliacha kazi ya JWTZ mwaka 1978,lakini baada ya kusikia Idd Amini amepindua nchi ya Uganda na kuvamia sehemu ya Kaskazini ya Tanzania aliamua kurudi jeshini kupambana na rafiki yake Idd Amin.

"Nilisema kama amevamia nchi yetu narudi jeshini,tulipambana naye,nilifika hadi kijijini kwake,Kampala pale alinusurika kuuawa, akatorokea njia ya Kenya,tuliwaomba Kenya wafunge mpaka walikataa hivyo Idd Amin akanusurika akatoroka ukawa ndiyo mwisho wa Vita ya Uganda''alisema.

Luteni Kanali Mstaafu Gangisa pia anasema alishirikiana na Samora Machel wa Msumbiji wakati wa harakati za kupigania Uhuru wa Msumbiji ambapo mara kadhaa amelala kwenye mashimo na Samora Machel.

Anasema Samora Machel mara baada ya Uhuru alifika Songea mwaka 1975 wakati anazungumza na wananchi alimshukuru Luteni Kanali Gangisa akisema

alishiriki naye kwa kutoa silaha na walilala wote kwenye mashimo na kula mihogo ya watu wakati wa mapambano ya wareno.

Gangisa anatoa rai kwa serikali kuwakumbuka wastaafu waliolitumikia Taifa kwa uzalendo mkubwa ili kumalizia kwa furaha maisha yaliobaki hapa duniani.

## WAZIRI MHAGAMA AWAFUNDA WAZAZI KUHUSU MALEZI BORA



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Mheshimiwa Jenista Mhagama amewataka wazazi kutenga muda wa malezi kwa watoto ili wawe na maadili mema.

Ameyasema hayo kwenye maadhimisho ya miaka 69 ya Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi yaliyofanyika katika Kijiji cha Kilagano Jimbo la Peramiho.

Waziri Mhagama amesema, mtoto anayelelewa kwa kuangalia mfano mzuri wa baba na mama atakuwa na nidhamu na tabia njema.

“Wazazi tutafakari utaratibu tunaotumia kulea watoto wetu ili wawe na madili bora katika katika Jamii,kizazi kipya kimeathirika na masuala ya utandawazi,nguvu mpya ya Mawasiliano isipotumika vizuri itakuwa ni chanzo cha upotofu wa maadili,” alisema Waziri Mhagama.

Amelitaja lengo la kuanzishwa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi ni kuhakikisha inajenga maadili mema ndani ya chama na taifa kwa ujumla.

## MADAKTARI BINGWA 40 WAANZA KUTOA HUDUMA ZA KIBINGWA RUVUMA




Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI inaendesha kampeni maalum ya kusogeza huduma za afya za kibingwa katika hospitali za Halmashauri 184 Tanzania Bara.

Hayo yamesemwa na Mwakilishi kutoka Wizara ya Afya Faraja Mgeni kwenye ufunguzi wa kambi ya matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi ya Dkt.Samia mkoani Ruvuma.

Madaktari bingwa 40 wameanza kutoa huduma za kibingwa katika Hospitali za Halmashauri zote nane mkoani Ruvuma,kuanzia Mei 6 hadi 10,2024

Mgeni amesema katika kipindi cha kuanzia Machi 2023 hadi kufikia Machi 2024 Wizara ya Afya kwa kushirikiana na TAMISEMI ilifanikiwa kuwajengea uwezo watoa huduma za afya Zaidi ya 4000 walioweza kutoa huduma za kibingwa kwa wananchi Zaidi ya 10,956.

“ ili kuimarisha huduma za afya kwa wananchi Wizara ya Afya na TAMISEMI inaendelea kuendesha kampeni maalum ya kusogeza huduma za afya za kibingwa katika hospitali za Halmashauri nchini,kampeni hii tunaianza leo Mei 6 na kukamilika Mei 28 mwaka huu na tutakuwa tumezifikia hospitali 184 zilizopo Tanzania bara’’,alisema.

Hata hivyo amesema katika Mkoa wa Ruvuma kampeni ya huduma za kibingwa inaanza Mei 6 na kukamilika Mei 10 mwaka huu na kwamba wananchi wanasogezewa huduma za kibingwa bobezi katika hospitali nane za Halmashauri mkoani Ruvuma.

Ametoa rai kwa Viongozi katika ngazi zote mkoani Ruvuma kushirikiana na madaktari bingwa hao na kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi ili kupata huduma hizo za kibingwa.

Kwa upande wake mgeni rasmi kwenye ufunguzi huo,Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed ambaye aliwakilishwa na Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Gilbert Simiya, ameipongeza serikali kwa kutoa madaktari bingwa na bingwa bobezi wa Dkt.Samia Suluhu Hassan ambao wamefika kutoa huduma za kibingwa mkoani Ruvuma.

Kanali Abbas ametoa rai kwa madaktari hao kufanya kazi yao kwa ufanisi mkubwa kwa kuwa serikali imeboresha upatikanaji wa vifaa tiba na kwamba serikali inaendelea kuboresha huduma za afya mkoani Ruvuma.

“Katika Mkoa wa Ruvuma serikali imetoa shilingi bilioni 18.721 kutekeleza miradi ya afya ikiwemo ujenzi wa hospitali ya Rufaa ya Mkoa,ujenzi wa hospitali za Halmashauri,vituo vya afya na zahanati’’,alisisitiza Kanali Abbas.

Ameitaja miradi mingine iliyotekelezwa mkoani Ruvuma ni ukarabati wa hospitali kongwe ya Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru,Mbinga Mji na ujenzi wa majengo ya huduma za dharura (EMD) katika hospitali za Tunduru,Nyasa,Madaba na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Dr.Louis Chomboko akizungumza kwenye ufunguzi huo amesema madaktari bingwa hao wanatekeleza mpango kabambe wa huduma za mkoba nchini lengo likiwa ni kuboresha huduma za kibingwa karibu na wananchi katika ngazi ya Halmashauri.

Amewataja madaktari bingwa hao wanatoka katika hospitali za rufaa za mikoa,hospitali za Kanda,hospitali ya Taifa na maalum na kwamba huduma za kibingwa zinazotolewa ni ubingwa wa akinamama na uzazi,Watoto,upasuaji,magonjwa ya ndani,utoaji dawa za ganzi na usingizi.

Kampeni hii ya ina kauli mbiu ya madaktari bingwa wa Rais Samia tumekufikia karibu tukuhudumie ambayo imelenga kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma za kibingwa katika Halmashauri zao ili kuwapunguzia gharama za kusafiri umbali mrefu.

## WAZIRI MHAGAMA AZINDUA MRADI WA BILIONI 3.1SONGEA




WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera,Bunge na Uratibu Mheshimiwa Jenista Mhagama amezindua mradi wa kuendeleza lishe na ufugaji endelevu wa viumbe maji kwa wakulima wadogo (ARSNA) unaogharimu shilingi bilioni 3.1 katika Kijiji cha Mpitimbi wilayani Songea mkoani Ruvuma.

Waziri Mhagama amesema mradi huo unaotekelezwa na serikali katika mikoa ya Ruvuma na Lindi kwa unafadhiliwa na serikali ya Norway kupitia Shirika la NORAD na kwamba unatekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia Machi 2024 hadi Machi 2026.

Ameutaja mradi huo kuwa umelenga kuleta mabadiliko makubwa kwenye uzalishaji na uendelezaji wa biashara ya ufugaji Samaki na uzalishaji wa mwani

kwa lengo la kuwawezesha wananchi kunufaika katika maeneo yao ufugaji Samaki na uzalishaji wa mwani.

Amesema serikali imekusudia kuendeleza kilimo na uvuvi katika mikoa ya Ruvuma,Lindi ili kupata mafanikio makubwa na kuongeza tija na kukabiliana na changamoto kubwa ya upatikanaji wa vifaranga vyenye ubora na chakula cha Samaki.

“Kupitia mradi huu wazalishaji binafsi wa vifaranga vya samaki watajengewa uwezo katika uzalishaji wa vifaranga na wafugaji wa Samaki hususan vijana watajengewa uwezo wa kutengeneza chakula cha Samaki ’’,alisisitiza Mhagama.

Waziri Mhagama amesema tayari serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imejenga shamba darasa la ufugaji wa samaki katika Kijiji cha Mpitimbi ambalo amesema litakuwa chachu kubwa katika ufugaji bora wa Samaki ambapo amewaomba wananchi hao kutumia shamba darasa hilo ili kuongeza tija katika ufugaji wa Samaki.

Ametoa rai kwa wakuu wa mikoa ya Ruvuma na Lindi ambako mradi huo unakwenda kutekelezwa kuhakikisha mradi unakwenda kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa ili kupata tija na thamani halisi ya fedha zitakazotumika.

Awali akitoa taarifa ya mradi huo Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera,Bunge na Uratibu Underson Mutatembwa ameutaja mradi wa ARSNA kuwa unataarajia kuzifikia kaya 5,000 za wakulima wadogo ikijumuisha wanawake asilimia 50 vijana asilimia 40 na makundi mengine asilimia 10.

Amesema mradi huo unaogharimu shilingi bilioni 3.1 unatekelezwa katika kipindi cha miaka miwili kuanzia Machi 2024 hadi Machi 2026 katika Halmashauri za Wilaya ya Songea na Mbinga mkoani Ruvuma na Halmashauri za Wilaya za Mtama na Ruangwa mkoani Lindi .

Amesema Tanzania imekuwa moja ya nchi tatu za Afrika zilizopata fursa ya kunufaika na utekelezaji wa mradi huu nchi nyingine amezitaja kuwa ni Msumbiji na Kenya na kwamba mradi huo ni sehemu ya utekelezaji wa program kubwa ya kuendeleza kilimo na uvuvi inayofadhiliwa na Shirika la IFAD inayotekelezwa katika mikoa 12 ya Tanzania kwa gharama ya shilingi bilioni 150.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo Mwakilishi wa Mkurugenzi IFAD Afrika Mashariki na Kusini Jacquiline Machangu amesema IFAD imekuwa ikifanya kazi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo sekta ya kilimo hususan wakulima wadogo waliopo vijijini.

Amesema IFAD kupitia mradi wa ARSNA imelenga kuongeza mapato na kujenga uwezo kimaisha wafugaji wadogo katika maeneo matatu.

Ameyataja maeneo hayo kuwa ni ongezeko la uzalishaji na ustahimilivu kwa wafugaji wadogo wa Samaki,kuongeza kwa fursa kwa wanawake na vijana kupitia ubunifu kwenye masoko na kuendeleza ujuzi na uundaji wa sera mpya.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Alexander Mnyeti akizungumza kwenye uzinduzi huo amesema Wizara hiyo itaendelea kutoa watalaam wa uvuvi ili kufanikisha mradi huo unakwenda kuzalisha Samaki wengi kwenye mabwawa ambao wana virutubisho muhimu.

Amesema Samaki wa mabwawa wanaweza kumaliza changamoto ya udumavu kwenye Mkoa wa Ruvuma ambapo hivi sasa udumavu umefikia asilimia 37 katika Mkoa wa Ruvuma , licha ya Mkoa huo kutajwa kuwa ni ghala la chakula nchini.



*Shamba darasa la ufugaji endelevu wa viumbemaji kwenye mabwawa ya Kijiji cha Mpitimbi wilayani Songea*

## TANROADS YAKAMILISHA KAZI YA KUIMARISHA DARAJA LA MUHUWESI



WAKALA wa barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Ruvuma,imekamilisha kazi ya kuimarisha daraja la mto Muhuwesi wilayani Tunduru ambalo liliathirika na mvua za masika na kusababisha taharuki kwa watumiaji wa daraja hilo.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Saleh Juma amesema,kwa sasa daraja hilo ni salama na haliwezi kusogea tena kama ilivyotokea hapo awali, na amewatoa hofu watumiaji hasa wenye magari kuhusu uimara wa daraja hilo linalounganisha mikoa ya Ruvuma,Lindi na Mtwara.

Amezitaja kazi nyingine zilizofanyika,ni kuziba mashimo makubwa kwenye barabara inayoingia katika daraja hilo yaliyosababishwa na maji ya mvua kupita chini ya barabara na kukatika kwa sehemu ya lami.

Amesema, katika eneo hilo barabara imemeza maji na kusababisha ifumuke,lakini tayari TANROADS kwa kumtumia Mkandarasi Kampuni ya Ovans Constructions Ltd imefanikiwa kuziba mashimo yaliyojitokeza.

“katika eneo hili magari yanayopita yalikuwa yanakwama na kusababisha adha kubwa,lakini tayari serikali kupitia TANROADS imefanya matengengezo ya haraka na sasa hali ni shwari”alisema.

Kwa upande wake Mhandisi wa Kampuni ya Ovans Constructions Ltd Azimio Mwapongo amesema, katika eneo hilo kulitokea changamoto ya maji kutokea chini kuja juu ya barabara na kusababisha lami kukatika.

Kwa mujibu wa Mwapongo,kazi zilizofanyika ni ulazaji wa mabomba chini ya ardhi kwa ajili ya kunyonya maji kutoka chini na kuyapeleka nje ili yasikae tena pamoja na kurudishia tabaka la lami.

## MILIONI 302 ZILIVYOBORESHA MAZINGIRA YA KUFUNDISHIA WENYE ULEMAVU TUNDURU



SERIKALI imetoa kiasi cha Sh.milioni 302 ili kuboresha mazingira na miundombinu ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi na walimu katika shule ya msingi Tunduru Mchanganyiko wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo Sabina Lupukila amesema,kati ya fedha hizo Sh.milioni 246 zimetoka serikali kuu na Sh.milioni 56 zimetolewa na Halmashauri ya wilaya Tunduru.

Lipukila amesema,Sh.milioni 80 zimetumika kujenga bweni,Sh.milioni 50 kujenga nyumba moja ya walimu ya familia mbili,Sh.milioni 60 kujenga uzio na Sh.milioni 56 kwa ajili ya matundu 32 ya vyoo.

Ameeleza kuwa,Sh.milioni 56 zilizotolewa na Halmashauri ya wilaya Tunduru, Sh.milioni 41 zimetumika kumaliza ujenzi wa miradi hiyo iliyoanzishwa na serikali kuu na Sh.milioni 15 kwa ajili ya kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Amesema, bweni lina uwezo wa kuchukua watoto 80 na katika awamu ya kwanza

litatumika kulala watoto wa kike wakati serikali ikiendelea na mchakato wa kujenga bweni lingine la watoto wa kiume.

Shule ya Tunduru Mchanganyiko ina wanafunzi 1,738 kati yao wanafunzi 43 ni wa elimu maalum kuanzia darasa la awali hadi la saba ambao wanatoka nyumbani na kwenda shule kila siku.

Hata hivyo amesema,ujenzi wa bweni hilo ni mpango wa serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dkt Samia Suluhu Hassan wa kuwajali watoto wenye mahitaji maalum na kuboresha mazingira ya elimu ili kuhamasisha watoto kupenda kusoma na wazazi kupeleka watoto wao shule kwa ajili kupata haki yao ya msingi.

“watoto wenye ulemavu sio kwamba hawana ndoto,lakini changamoto kubwa imetokana na mazingira magumu kwa baadhi ya wazazi,natoa wito kwa wazazi na walezi wote wenye watoto wenye mahitaji maalum wawalete watoto wao kwenye shule hii”alisema.

Mratibu elimu Kata ya Mlingoti Mashariki Erith Banda,ameishukuru serikali kujenga bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum na nyumba moja ya kuishi walimu. Ambilikile Mwandembo Mwalimu wa watoto wenye ulemavu amesema,watoto hao wamegawanyika kwenye makundi matatu ambayo ni wenye ulemavu wa akili,wenye ulemavu wa kusikia,wenye uono hafifu na wenye ulemavu wa ngozi.

## UZINDUZI MRADI WA UFUGAJI SAMAKI MPITIMBI



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera,Bunge na Uratibu) Mheshimiwa Jenista Mhagama amezindua mradi wa kuongeza ustahimilivu na lishe kwa wafugaji wadogo wa samaki unaogharimu zaidi ya shilingi bilioni tatu ambao unatekelezwa katika kijiji cha Mpitimbi Halmashauri ya Wiaya ya Songea mkoani Ruvuma.Mradi huu umelenga kupunguza umaskini na kuboresha lishe kupitia shughuli za ufugaji wa samaki wenye tija na ustahimilivu kutoka kwa wazalishaji na wafugaji wadogo ikiwemo kuwajengea uwezo kimaisha wafugaji wadogo wa samaki waliopo vijijini

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera,Bunge na Uratibu) Mheshimiwa Jenista Mhagama amezindua mradi wa kuongeza ustahimilivu na lishe kwa wafugaji wadogo wa samaki unaogharimu zaidi ya shilingi bilioni tatu ambao unatekelezwa katika kijiji cha Mpitimbi Halmashauri ya Wiaya ya Songea mkoani Ruvuma.Mradi huu umelenga kupunguza umaskini na kuboresha lishe kupitia shughuli za ufugaji wa samaki wenye tija na ustahimilivu kutoka kwa

wazalishaji na wafugaji wadogo ikiwemo kuwajengea uwezo kimaisha wafugaji wadogo wa samaki waliopo vijijini




Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera,Bunge na Uratibu) Mheshimiwa Jenista Mhagama amezindua mradi wa kuongeza ustahimilivu na lishe kwa wafugaji wadogo wa samaki unaogharimu zaidi ya shilingi bilioni tatu ambao unatekelezwa katika kijiji cha Mpitimbi Halmashauri ya Wiaya ya Songea mkoani Ruvuma.Mradi huu umelenga kupunguza umaskini na kuboresha lishe kupitia shughuli za ufugaji wa samaki wenye tija na ustahimilivu kutoka kwa wazalishaji na wafugaji wadogo ikiwemo kuwajengea uwezo kimaisha wafugaji wadogo wa samaki waliopo vijijini

# WANANCHI RUVUMA WANAVYONUFAIKA NA MADAKTARI BINGWA



Huduma za mkoba za madaktari Bingwa zinatarajia kuanza kutolewa katika hospitali za Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma kuanzia Mei sita hadi 10 mwaka huu.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Dr.Louis Chomboko amesema timu ya madaktari bingwa 40 ipo mkoani Ruvuma na inatarajia kuripoti kwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed Mei 6 mwaka huu kabla ya Kwenda kuanza kazi ya kutoa huduma katika hospitali za Halmashauri.

Dr.Chomboko amewataja madaktari Bingwa ambao wapo mkoani Ruvuma kwa ajili ya kuanza kutoa huduma za kibingwa ni Pamoja na madaktari wa magonjwa ya wanawake na uzazi,madaktari bingwa wa Watoto na Watoto wachanga,madaktari bingwa wa magonjwa ya ndani,madaktari bingwa wa upasuaji na wabobezi wa mfumo wa mkojo na madaktari bingwa wa usingizi na ganzi.

Amezitaja hospitali ambazo madaktari hao watatoa huduma hizo ni Pamoja na hospitali ya Halmashauri ya wilaya ya Namtumbo,Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Mbinga,Hospitali ya Halmashauri ya Madaba na Hospitali ya Halmashauri ya Songea iliyopo Mpitimbi.

Hospitali nyingine amezitaja kuwa ni hospitali ya Wilaya ya Tunduru,hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga na kituo cha Afya Mji Mwema kilichopo Manispaa ya Songea.

Natoa rai kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kujitokeza katika hospitali hizo kupata huduma za kibingwa ,serikali imewasogezea madaktari bingwa kwenye maeneo yenu hivyo kuwapunguzia gharama za kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za kibingwa,mgonjwa anaweza kutumia bima au fedha taslimu'',alisema Dr.Chomboko.

## MAADHIMISHO YA KIMATAIFA YA FAMILIA KUFANYIKA NAMTUMBO



KAMATI ya Maandalizi kuelekea siku ya kimataifa ya familia ya Mkoa wa Ruvuma ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mchungaji Elimu Mwenzegule imedhamiria kuanza kutoa elimu rasmi kwa jamii kupitia majukwaa mbalimbali kuanzia Mei 6 hadi Mei 15 mwaka huu.

Kilele cha maadhimisho ya siku ya kimataifa ya familia katika Mkoa wa Ruvuma kinatarajia kufanyika wilayani Namtumbo Mei 15 mwaka huu ambapo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed.

Mchungaji Mwenzegule amesema Kamati hiyo katika mwezi huu inatarajia kutoa elimu kupitia redio za jamii,kutoa elimu kwa wanafunzi katika shule 16 za msingi na sekondari,kutoa elimu katika misikiti na makanisa na kutoa elimu kwenye mikusanyiko ya watu.

Kamati hiyo katika maadhimisho ya mwaka huu intarajia kutoa elimu kwa jamii kuhusu malezi chanya ya Watoto na familia kwa kuimarisha uelewa wa malezi na matunzo ya Watoto na wajibu wa wazazi na walezi katika malezi ya Watoto na familia.

Kaulimbiu ya maadhimisho ya siku ya kimataifa ya familia mwaka huu inasema "*Tukubali tofauti zetu kwenye familia,kuimarisha malezi ya Watoto*".

Kaulimbiu hiyo inawahimiza wazazi na walezi umuhimu wa kumaliza tofauti zao,kudumisha upendo na amani katika familia kwa sababu mifarakano katika familia ina athari kubwa kwenye malezi na makuzi ya Watoto.

Taarifa ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii,Jinsia na Wanawake na Makundi Maalum inaonesha kuwa katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 jumla ya familia 14,600 zilitoa taarifa Ofisi za Ustawi wa Jamii kuwa na migogoro katika ndoa na mahusiano ya wenza.

Idadi hiyo ya taarifa ni kubwa hivyo inahitajika nguvu ya Pamoja kutoka katika jamii nzima ili kuleta mabadiliko na kupunguza changamoto za malezi na makuzi ya Watoto.



## SERIKALI YATOA MILIONI 434 KUJENGA STENDI MPYA PERAMIHO




Serikali imetoa Zaidi ya shilingi milioni 434 kutekeleza mradi wa ujenzi wa stendi hiyo.Mradi wa stendi hiyo una jumuisha Jengo la Utawala, Maduka 36, Vibanda vya walinzi viwili, vyoo matundu nane  pamoja na uzio

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma,Kanali Ahmed Abbas Ahmed baada ya ukaguzi wa stendi hiyo amepongeza usimamizi mzuri wa mradi huo ambao umefanywa kwa kushirikiana na wananchi na watendaji.



## SOKO LA MADINI TUNDURU KUFANYIKA KATIKA ENEO MOJA




Mkuu  wa Wilaya ya Tunduru mkoani Mheshimiwa Simon Kemori Chacha, amewataka wafanyabiashara wa madini ya vito wilayani humo kufanyakazi katika eneo moja la biashara lililotengwa.

Agizo hili limetolewa katika kikao kilichofanyika na wafanyabiashara hao kwenye eneo linalojengwa soko la kimataifa la madini ya vito wilayani Tunduru.

Mheshimiwa Chacha amesisitiza umuhimu wa ushirikiano miongoni mwa wafanyabiashara hao ili kukuza sekta ya madini ya vito.

Amewataka wafanyabiasha hao kufanya kazi pamoja katika eneo lililotengwa ambalo litakuwa rahisi  kusimamiwa na serikali.

“Tunatambua umuhimu wenu katika kukuza uchumi hususani katika Wilaya yetu ,tunaamua kuboresha miundombinu ili kukuza sekta ya madini”. alisema Chacha.

Mheshimiwa Chacha, ametoa wito kwa wadau kuunga mkono mradi huu muhimu kwa ya ajili ya maendeleo ya wilaya ya Tunduru na Taifa kwaujumla.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru Chiza Marando amesema ,ujenzi wa soko la kimataifa la madini ya vito,unaendelea vizuri ambapo amesema soko hilo litatoa mazingira bora kwa wafanyabiashara hao .

## WWF KUBORESHA UHIFADHI NA UTALII RUVUMA



Katikati ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed akiwa katika picha ya pamoja na wataalam wa WWF wanaofanya kazi katika ushoroba wa Selous-Niassa .wataalam hao wamedhamiria kuendeleza sekta ya uhifadhi na utalii mkoani Ruvuma.Mwenye nguo nyekundu ni Katibu Tawala Mkoa wa Ruvuma Rehema Madenge

## MBUNGE WA MADABA AWAPIGA JEKI WANAFUNZI WA LILONDO



MBUNGE wa Jimbo la Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma Dkt. Joseph Mhagama ameweka umeme wa jua katika shule mpya ya Sekondari Lilondo iliyopo kata ya Wino iliyojengwa kwa shilingi Milioni 560.

Akizungumza kwa niaba ya Mbunge wa Jimbo hilo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Madaba Mheshimiwa Teofanes Mlelwa amesema umeme huo wa jua umewekwa kwa muda ikiwa jitihada za kupeleka umeme wa TANESCO zinafanyika ili kuhakikisha wanafunzi walioanza kidato cha kwanza mwaka huu 2024 wanasoma katika mazingira rafiki.

Kwa upande wake Mkuu wa Shule ya Sekondari Lilondo Subira Mapunda amemshukuru Mbunge wa Jimbo hilo kwa msaada huo ambao utasaidia wanafunzi hao katika masomo yao

## SERIKALI YATOA MAGARI MAWILI YA KUBEBEA WAGONJWA MADABA



SERIKALI ya Awamu ya Sita imetoa magari mawili ya kubebea wagonjwa katika Halmashauri ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma.

Katibu Tawala Wilaya ya Songea Mtela Mwampamba amekabidhi magari hayo kwa Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Mheshimiwa Teofanes Mlelwa.

Mwampamba amewaagiza madereva watakaoendesha magari haya kuyatunza ili yaweze kutumika kwa muda mrefu.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Mheshimiwa Mlelwa amemshukuru Rais Samia kwa kuleta magari hayo ambayo yatawasaidia wananchi kupata urahisi wa matibabu.




*Jengo la Halmashauri ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma*

# TAKUKURU RUVUMA ILIVYOCHUNGUZA MIRADI 15 YA BILIONI 10




Taasisi ya Kuzuia na Kapambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Ruvuma imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake katika robo ya Januari hadi Machi 2024,kwa kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo 15 yenye dhamani ya shilingi bilioni kumi.

Hayo yamebainishwa na Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma Janeth Haule, wakati akitoa taarifa ya utendaji kazi wa TAKUKURU kwa wanahabari kwenye ukumbi wa Taasisi hiyo iliyopo Mahenge mjini Songea.

Haule amesema ufuatiliaji huo umefanyika katika miradi ya ujenzi wa madarasa na vyoo katika shule mpya za msingi na sekondari,ukarabati wa mabweni na chumba cha maabara zilizoko katika halmashauri za wilaya tano,miradi ikiwa na thamani ya shilingi 3,449,954,835.60

Amesema katika kipindi hicho wamefuatilia ujenzi wa nyumba za watumishi ikiwemo nyumba ya Mkurugenzi na Wakuu wa idara wa Halmashauri ya Mbinga ,ujenzi wa nyumba za waalimu katika Halmashauri ya Namtumbo na Tunduru zenye thamani ya shilingi 838,859,638/=

Ameongeza kuwa TAKUKURU pia wamefuatilia ujenzi wa miundombinu wa miradi ya maji katika Halmashauri Wilaya ya Nyasa na Halmashauri Wilaya ya Tunduru yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 6.8

Hata hivyo amesema TAKUKURU iligundua mapungufu katika miradi miwili yenye thamani ya sh. 4,822,986,357.83/=

TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma inatoa wito kwa wananchi kuendelea kuunga mkono jitihada za kufichua vitendo vya Rushwa kwa kutoa taarifa sahihi ili wachukuliwe hatua husika hasa katika kipindi hiki cha uchaguzi wa serikali za mitaa.

## SERIKALI ILIVYOBORESHA MAJENGO HOSPITALI YA TUNDURU



SERIKALI imetoa shilingi milioni 900 kufanya ukarabati majengo ya hospitali kongwe ya wilaya ya Tunduru mkoanI Ruvuma pamoja na kununua vifaa tiba hali ambayo imeboresha huduma za afya zinazotolewa katika hospitali hiyo.



## WATUMISHI RUVUMA WALIVYOADHIMISHA MEI MOSI KIMKOA TUNDURU



Siku ya wafanyakazi Mkoani Ruvuma imeazimishwa katika Wilaya ya Tunduru ambapo vyama vya wafanyakazi vimepaza sauti zao kulalamikia Serikali kuhusu kikokotoo Kilichopo Kwa watumishi wa umma wakati wa kustaafu.

Akisoma Risala ya wafanyakazi Kwa Mgeni Rasmi katibu wa TUGHE Mudathiri Ismail ambaye pia ni Mratibu wa Maadhimisho hayo amesema kikokotoo hakiwahusu waajiriwa wa zamani Kwa kuwa hakikuwa katika mikataba Yao ya ajira.

Ismail katika Risala hiyo amedai wafanyakazi wanafanya tathmini ya hatima ya ajira zao wakikinyoshea kidole kikokotoo ambacho kina watesa wafanyakazi hao wanapostaafu baada ya kuitumikia serikali kwa uaminifu mkubwa .

Hata hivyo Ismail amesema kuwa mishahara ya wafanyakazi bado haikidhi mahitaji ukilinganisha na gharama halisi za maisha hivi Sasa .

Mgeni Rasmi katika Maadhimisho hayo Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed Pamoja na mambo mengine amevishukuru vyama vya wafanyakazi Kwa kuandaa Maadhimisho hayo ya Mei Mosi na kujitokeza Kwa wingi kuhudhuria Maadhimisho hayo.

Kanali Abbas amewataka waajiri katika Mkoa wa Ruvuma kujenga mazoea ya kutoa zawadi mara kwa mara Kwa wafanyakazi ili kuongeza morali ya kufanyakazi Kwa watumishi badala ya kusubiri siku ya wafanyakazi pekee.

Mkuu wa Mkoa ameitaja migogoro ya wafanyakazi inatokana na kutozingatia misingi ya utawala Bora ,kutokuwa na ushirikishwaji, usiri usio wa lazima na uamuzi usiozingatia haki Kwa watumishi.

Hata hivyo amewapongeza wafanyakazi kupitia Risala yao kuthamini kazi kubwa ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt .Samia Suluhu Hassan katika ujenzi wa miradi mbalimbali Mkoani Ruvuma .

Kanali Abbas amewahakikishia wafanyakazi kuwa Changamoto zote zilizotolewa zimepokelewa na ofisi yake na Changamoto zinazoweza kutatuliwa na ofisi yake zitafanyiwa hivyo na zingine zitapelekwa katika ngazi ya kitaifa.

Maadhimisho ya siku ya wafanyakazi mwaka huu yamebeba kauli Mbiu isemayo "Nyongeza ya mishahara ni msingi wa mafao bora na kinga dhidi ya hali ngumu ya maisha.

## RC RUVUMA AWAAPISHA WAJUMBE WA BARAZA LA ARDHI



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas amewaapisha wajumbe wanne wa Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Namtumbo.

Wajumbe hao walioapishwa katika hafla iliyofanyika katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa mjini Songea ni pamoja na Kisuu Mtimda,Longinus Mhagama,Fatuma Mapunda na Mecktilda Chiwango .

Wajumbe hao wataliongoza Baraza hilo kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia Aprili 30,2024.

Akizungumza baada ya kuwaapisha wajumbe hao Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma amewapongeza kwa kupata nafasi hiyo ambapo amewataka kutenda haki bila upendeleo .

"Wilaya zina migogoro mingi ya ardhi,mabaraza ya ardhi kazi yake ni kufanya usaidizi ili kupunguza changamoto za migogoro ya ardhi katika wilaya ",alisisitiza.

Kanalı Abbas ameshauri kila Mjumbe kuhakikisha anatenda haki kulingana na kiapo chake.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Songea Ismail Ayo amesema wajumbe hao wameapishwa kwa mujibu wa kanuni za Baraza la Ardhi na Nyumba la wilaya za mwaka 2003 .

Ayo amesema wananchi wa Namtumbo hivi sasa wataepuka aza kubwa kusafiri hadi Songea kufuata huduma ya Baraza la Ardhi na Nyumba.

## MADAKTARI BINGWA WAWEKA KAMBI YA SIKU TANO HOMSO




Timu ya madaktari Bingwa kutoka mikoa ya Ruvuma,Songwe na Mbeya wameanza kutoa huduma za uchunguzi na matibabu ya magonjwa mbalimbali kwa wananchi wa mkoa wa Ruvuma.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Dr. Louis Chomboko amesema ,kambi ya Madaktari bingwa katika Mkoa wa Ruvuma itakuwa ya siku tano kuanzia Aprili 29 hadi Mei 4 mwaka huu.

Naye Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Songea (HOMSO)Dr.Majura Magafu amesema,uchunguzi na matibabu hayo yatahusisha magonjwa ya akina Mama,magonjwa ya ndani kama vile shinikizo la damu,kisukari na figo.

Dr. Majura ameyataja magonjwa mengine yatakayochunguzwa ni magonjwa ya watoto,mifupa,upasuaji,macho,kinywa,meno,upasuaji wa midomo sungura, masikio,pua,koo,afya ya akili,ngozi,moyo,mfumo wa chakula na saratani.

Amesema, Wizara ya Afya na TAMISEMI inaendelea kuboresha huduma za kibingwa na ubingwa bobezi kwa kuwatumia madaktari waliopo katika Hospitali za rufaa za mikoa,kanda,taasisi na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Kwa mujibu wa Dr. Majura,lengo kuu la kuwatumia madaktari bingwa waliopo katika Hospitali na taasisi za serikali ni kufikisha matibabu ya kibingwa kwa wananchi wengi na kwa wakati ili zisaidie wanannchi kupata huduma bora na kwa gharama nafuu.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanal Ahmed Abbas Ahmed ameipongeza serikali kwa kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kuboresha huduma za afya katika maeneo mbalimbali ikiwemo katika mkoa wa Ruvuma.

Amewataka Madaktari Bingwa,kutowasubiri wagonjwa hadi wafike Hospitali badala yake, wahakikishe wanajikita zaidi katika kutoa elimu inayohusiana na madhara,namna ya kujikinga na pia kuwafuata wananchi waliko jambo litakalowezesha kuwafikia watu wengi.

Amesema serikali itaendelea kuwekeza kwa kutoa fedha na kuajiri wataalam kwa ajili ya kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Rehema Madenge,ametoa wito kwa wananchi kutumia fursa za kambi hiyo kupata huduma za kibingwa kwa gharama nafuu na kupunguza usumbufu wa kufuata huduma mbali na maeneo yao.



## WAWEKEZAJI WANAENDELEA KUKARIBISHWA RUVUMA



Mkoa wa Ruvuma umebarikiwa kuwa na fursa mbalimbali za uwekezaji katika sekta mbalimbali hali ambayo inachochea maendeleo ikiwemo kutoa ajira kwa vijana.Huu ni ukumbi wa  hoteli ya one Pasific uliojengwa mjini Mbinga ambayo ni miongoni mwa kumbi zinazovutia wadau wengi kutumia miundombinu bora ya kuvutia iliyopo .Mkoa wa Ruvuma unatarajia kuona wawekezaji wengi wa ndani na nje kujitokeza kuwekeza katika sekta mbalimbali ndani ya Mkoa wa Ruvuma



## MAADHIMISHO YA SIKU YA MKULIMA NAMTUMBO



Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo Mheshimiwa Ngollo Malenya akizungumza kwenye maadhimisho ya siku ya mkulima yaliyofanyika kwenye viwanja vya Wakala wa Mbegu za Kilimo ASA wilayani Nanmtumbo ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed



## RUVUMA KITUO CHA PILI KWA UKUBWA UZALISHAJI MBEGU BORA NCHINI



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed ameipongeza serikali kupitia Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) kwa kuuwezesha Mkoa kuwa kituo cha pili kwa ukubwa hapa nchini kwa uzalishaji wa mbegu bora.

Akizungumza kwenye maadhimisho ya siku ya mkulima yaliyofanyika katika viwanja vya ofisi ya shamba la mbegu Namtumbo linalomilikiwa na ASA,Kanali Abbas amelitaja shamba hilo la kuzalisha mbegu kuwa ni la pili kwa kubwa nchini likiwa na hekta 3,580.4.

“Hii ni fursa kubwa kwetu tulioendelea kupewa na Taifa,licha ya Mkoa wa Ruvuma kuwa wazalishaji wa kwanza nchini wa mazao ya chakula na nafaka ,bado Mkoa umeendelea kupata heshima ya kuwa ni kituo cha uzalishaji mbegu wa mbegu bora cha pili kwa ukubwa ndani ya Taifa letu’’,alisisitiza Kanali Abbas.

Ameipongeza Wizara ya Kilimo kwa kuamua kulirudisha shamba la NAFCO Namtumbo kuwa miongoni mwa mashamba ya serikali yanayozalisha mbegu bora ambazo zitaongeza uzalishaji mazao ya chakula na serikali kujihakikishia usalama wa chakula.

Ameongeza kuwa mbegu bora zinazozalishwa kwenye kituo hicho zitapatikana kwa gharama nafuu na kwamba mradi huo umetoa fursa kwa wawekezaji wa

kilimo cha mkataba ambapo ameiagiza ASA kuhakikisha wanapatikana wawekezaji wengi wa mkataba ili shamba hilo lisibaki kuwa mapori.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma ametoa rai kwa ASA kuhakikisha wanafanya kilimo cha kisasa kwa kuondokana na kilimo cha matumizi ya vifaa duni badala yake kuongeza kasi ya kutumia vifaa vya kisasa.

## UVUVI UNAVYOCHANGIA PATO LA WANANCHI WA NYASA



MOJA ya shughuli kubwa inayowaingizia mapato wananchi wa Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma ni uvuvi katika ziwa Nyasa.Ziwa Nyasa linatajwa kuwa na aina mbalimbali za samaki wakiwemo samaki wa mapambo.wananchi wa Nyasa hupata chakula na fedha kupiitia samaki wanaovuliwa katika ziwa Nyasa



## SHAMBA LA MBEGU BORA NAMTUMBO KUIMARISHA SEKTA YA KILIMO



Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) Dkt.Sophia Kashenge akizungumza kwenye maadhimisho hayo amelitaja shamba la mbegu Namtumbo lenye ukubwa wa hekta 3,580.4 kuwa ni miongoni mwa mashamba 16 ya mbegu yenye jumla ya hekta 17,710.26.

Ameyataja mashamba hayo ya mbegu yanapatikana katika mikoa ya Morogoro, Iringa, Ruvuma, Tanga, Pwani, Arusha, Tabora, Kigoma,Katavi na Geita na kwamba shamba la mbegu Namtumbo ni la pili kwa ukubwa hapa nchini likiwa na watumishi 15.

Amesema katika msimu wa mwaka 2023/2024,shamba la mbegu Namtumbo linatarajia kuzalisha mbegu Zaidi ya tani 1,275 za mazao mbalimbali yakiwemo mahindi na alizeti .

**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA SEKRETARIETI YA MKOA WA RUVUMA**

**Kupitia Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma**

# ANWANI NA MAWASILIANO



**S.L.P 74 SONGEA**
**57180 RUVUMA**
**SIMU 025- 2602256/2602238**
**FAX Na.2602144**
**E-MAIL: ras.ruvuma@tamisemi.go.tz**
**TOVUTI: www.ruvuma.go.tz**
**INSTAGRAM; rs ruvuma**
**FACEBOOK: rs ruvuma**
**YOUTUBE: rs ruvuma**